Appendix D: Draft Order (Swahili Version)

Ombi la Kurekebisha Bei za Majisafi na Majitaka la

MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA (BUWASA)

Utangulizi

1. Tarehe 22 Juni, 2011, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji ("EWURA") ilipokea ombi kutoka BUWASA kuhusu mambo sita yafuatayo:

(a) kuongeza bei ya maji kwa wateja wa majumbani wenye mita kwa kiwango cha asilimia 17 hadi 20, kwa wateja wa taasisi kutoka asilimia 15 hadi 17, wateja wa biashara kutoka asilimia 14 hadi 18, wateja wa viwanda kutoka asilimia 25 hadi 27 na kwa wateja wa maghati kwa asilimia 33;

(b) kuanzisha namna mpya ya kutoza tozo kwa wateja wasio na dira ambayo itazingatia makisio ya matumizi halisi kwa bei ya wateja wenye dira katika makundi husika;

(c) kuendelea na bei gharama za sasa za kuunganisha wateja wapya;

(d) kuongeza gharama za kurejeshewa huduma ya maji kwa wateja wa makundi yote kwa asilimia 100;

(e) kuongeza tozo ya huduma kwa wateja wote kwa asilimia 25; na

(f) kuongeza tozo ya dira kwa wateja wa makundi yote kwa asilimia 25.

Ushirikishwaji wa Wadau

2. Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2)(h) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414, EWURA ilifanya taftishi kuhusu uhalali wa ombi la kurekebisha bei za huduma ya maji za BUWASA. Taftishi hiyo ilihusisha tathmini ya masuala ya kiuchumi na ya kiufundi pamoja na kufanya mkutano wa taftishi tarehe 6 Oktoba 2011 katika mji wa Bukoba ili kusikia maoni ya wadau.

3. Wakati wa mkutano wa taftishi, BUWASA iliwasilisha mada juu ya ombi lake ikielezea sababu na uhalali wa mapendekezo ya nyongeza ya bei na gharama. Wadau wote wakiwemo wateja wa BUWASA, Baraza la Ushauri la Serikali (*Government Consultative Council* ("GCC")), na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA (*Consumers Consultative Council* ("CCC")) walipata fursa ya kuchunguza

na kutoa maoni yao kuhusiana na uhalali wa ombi hilo. BUWASA vile vile ilipewa fursa ya kujibu hoja za wadau kwenye mikutano hiyo na kuwasilisha EWURA majibu ya hoja za wadau kwa maandishi.

4. Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji lilihoji, pamoja na mambo mengine, gharama kubwa ya uendeshaji, ufanisi mdogo kwenye makusanyo ya ankara, ubora wa maji na kwenye utoaji wa huduma.

5. GCC walihoji, pamoja na mambo mengine, upotevu mkubwa wa maji, kuongezeka kwa asilimia ya wateja wasio na dira, kutokuwepo na mpango wa ukarabati na kutokuwepo na uwazi juu ya miradi ya uwekezaji ya Wafadhili na Serikali.

6. Kutoka kwa wateja wa BUWASA, kulikuwa na malalamiko juu ya kukosekana kwa maji maeneo ya Kitendaguro, kutokuwepo na huduma ya majitaka, kuchelewa kukarabati mabomba yanayovuja pindi taarifa inapotolewa na kutoeleweka dhana ya tozo la huduma

7. Wakati wa kuhitimisha taftishi tarehe 20 Oktoba 2011, BUWASA iliweza kujibu hoja za wadau kwa kiasi cha kuridhisha; na EWURA ilikusanya taarifa za kutosheleza kufanya maamuzi. Wakati wa uchambuzi wa ombi, BUWASA ilitakiwa, na ilitoa maelezo ya ziada kuhusu ombi hilo

Uchambuzi na marekebisho

8. Kufuatia kukamilika kwa taftishi hiyo, EWURA imefikia uamuzi kwamba ombi la nyongeza ya bei lina mantiki na ni halali, isipokuwa kwa marekebisho madogo yaliyofanyika kwenye kasma ya utawala. .

Maamuzi

9. Maombi na marekebisho ya mahitaji ya mapato ya BUWASA ni kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali hapa chini

Jedwali 1: Mahitaji ya Mapato

MAPATO YA UENDESHAJI NA MENGINEYO	**Mapendekezo ya Mapato, 2011/12**	**Mapato Yaliyoidhinishwa, 2011/12**
	TZS	**TZS**
Mapato ya Maji	1,167,907,440	1,167,907,440
Mapato mengine ya uendeshaji	366,488,500	334,358,800
Jumla ya mapato ya uendeshaji	**1,534,395,940**	**1,502,266,240**
Mapato mengineyo		
Ruzuku kutoka serikalini	1,354,395,940	1,322,266,240
Uchakavu (Amortization of Grants)	7,265,350,000	7,265,350,000
Mauzo ya tenda	180,000,000	180,000,000
JUMLA YA MAPATO	**7,445,350,000**	**7,445,350,000**
GHARAMA ZA UENDESHAJI NA MATENGENEZO		
Uzalishaji Maji	192,107,500	192,107,500
Usambazaji	40,910,000	40,910,000
Marekebisho na Matengenezo	98,580,000	98,580,000
Rasilimali Watu	522,115,120	522,115,120
Utawala	252,493,900	251,008,900
Ukuzaji wa Biashara	38,098,000	38,098,000
Matukio na Michango	12,800,000	12,800,000
Ada mbalimbali	36,279,074	36,279,074
Gharama za Kifedha	5,700,000	5,700,000
Total O&M Expenses	**1,199,083,594**	**1,197,598,594**
Uchakavu	300,000,000	300,000,000
JUMLA MAHITAJI YA MAPATO	**1,499,083,594**	**1,497,598,594**

10. Katika kikao chake cha tarehe 16 Desemba 2011, Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA ilijadili ombi la BUWASA na kutoa maamuzi kama inavyoonyeshwa kwenye Agizo hapa chini:

SHERIA YA MAJISAFI NA MAJITAKA

(SURA NA 272)

AGIZO Na. 11-018

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d)cha Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, 2009)

MAMLAKA YA MAJISAFI NA MAJITAKA BUKOBA ("BUWASA"), AGIZO LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI, 2011

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba ("BUWASA") Agizo la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji, 2011 na litaanza kutumika tarehe 1 Januari, 2012.

Marekebisho ya Bei

2. Bei za maji za Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Bukoba ("BUWASA") zinarekebishwa kulingana na majedwali yaliyopo katika Agizo hili.

3. Bei zilizopitishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Ifikapo tarehe 30 Juni 2012 aub kabla ya hapo, BUWASA inatakiwa:

(i) kupunguza kiwango cha maji yanayopotea kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 47 hadi asilimia 30 au chini ya hapo, na

(ii) kuboresha programu ya kompyuta ya kukusanya mapato ili iweze kutambua malipo yanayofanyika baada ya kufunga mwezi;

Masharti

(b) Ifikapo tarehe 30 Juni 2012 au kabla, BUWASA iwe imewafungia wateja wake wote dira za maji kwa kutumia sehemu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya uchakavu;

(c) ifikapo au kabla ya tarehe 30 Juni 2012, BUWASA, kwa kufuata mwongozo uliotolewa na EWURA, itawasilisha EWURA marejeo ya Mpango wake wa Biashara (Business Plan), Mpango wa Fedha wa muda mrefu (Longterm Financial Plan) na Mpango wa Usimamizi wa Mali na Rasilimali (Asset Management Plan); na

(d) BUWASA itaendelea kuwasilisha kwa EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa mwongozo wa EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa BUWASA ikilinganiswa na Mamlaka nyingine za Majisafi na Majitaka nchini. EWURA itazingaitia tathmini hii

katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na BUWASA katika siku zijazo.

Utenguzi

4. Agizo Na. 10-018 la tarehe 3 Oktoba 2008 la Marekebisho ya Bei za Maji za Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Bukoba linatenguliwa.

KIAMBATANISHO

Jedwali 1: Bei za Wateja Wenye Dira za Maji

Kundi	**Matumizi ya Maji m^3**	**Bei ya Sasa TZS/m^3**	**Bei Iliyoidhinishwa TZS/m^3**
Majumbani	0-5	545	650
	>5-10	554	665
	>10	577	675
Taasisi	0-5	629	725
	>5-10	643	750
	>10	671	785
Biashara	0-5	639	730
	>5-10	648	755
	>10	676	795
Viwanda	0-5	704	880
	>5-10	714	895
	>10	732	930
Magati (DPs)		376	TZS10/20Lt

Jedwali 2: Bei kwa Wateja Wasio na Dira za Maji

Kundi	**Bei Iliyoombwa**	**Bei Iliyoidhinishwa**
Makundi yote ya Wateja	Malipo kulingana na matumizi ya maji kwa kuzingatia bei iliyoidhinishwa kwa wateja wenye dira kwa kila kundi la wateja	Malipo kulingana na matumizi ya maji kwa kuzingatia bei iliyoidhinishwa kwa wateja wenye dira kwa kila kundi la wateja

Jedwali 3: Tozo ya Kujiunga (Mteja Mpya)

Kundi	**Bei ya Sasa (TZS/Unganisho)**	**Bei Iliyoidhinishwa (TZS /Unganisho)**
Majumbani	15,000	15,000
Taasisi	20,000	20,000
Biashara	25,000	25,000
Viwanda	100,000	100,000

Jedwali 4: Ada ya Kurejesha Huduma

Kundi	**Bei ya sasa (TZS/Unganisho)**	**Bei Iliyoidhinishwa (TZS /Unganisho)**
Majumbani	5,000	10,000
Taasisi	10,000	20,000
Biashara	15,000	30,000
Viwanda	30,000	60,000

Jedwali 5: Ada ya Kubadilisha Maungio ya Maji

Kundi	**Bei ya Sasa (TZS/Mwezi)**	**Bei Iliyoidhinishwa (TZS /Mwezi)**
Majumbani	800	1,000
Taasisi	920	1,150
Biashara	1,060	1,325
Viwanda	1,800	2,250

Jedwali 6: Tozo ya Dira

Ukubwa wa Dira	**Bei ya Sasa (TZS/Mwezi)**	**Bei Iliyoidhinishwa (TZS /Mwezi)**
½" - ¾"	800	1,000
1" – 1½"	1,800	2,250
2"	5,600	7,000
4"	8,600	10,750

HARUNA MASEBU
Mkurugenzi Mkuu
EWURA
Dar es Salaam
16 Desemba 2011